**Augustine Lwehumbiza Kamuzora, (1915–2012)**

Augustine Lwehumbiza Kamuzora alikuwa mlei aliyejitolea ambaye alianzisha vuguvugu la uanzishwaji na upandaji wa makanisa mapya katika wilaya za Bukoba, Karagwe, Muleba, Misenyi, Geita, na Sengerema katika wilaya za upande wa Magharibi mwa Tanzania. Yeye amekuwa nguzo katika maendeleo ya Uadventista mkoani Kagera.

**Maisha ya Awali, Uongofu, na Elimu**

Inaaminika kuwa Augustine Lwehumbiza Kamuzora alizaliwa kati ya Juni 21 na 23, 1915, siku ambayo Waingereza walishambulia kwa bomu mji wa Bukoba wakati wa Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, kijijini kwao Kigarama katika kata ya Kanyigo wilayani Missenyi mkoani Kagera, nchini Tanzania. Baba yake alikuwa Michael Kamuzora Lwabusimbi, na mama yake alikuwa Martha Lutegaisa Nyamichwo. Wazazi wake walikuwa Banyoro kutoka Uganda. Augustine Lwehumbiza Kamuzora alikuwa mtoto wa tano katika familia ya watoto saba.

Augustine alitumia utoto wake katika kijiji cha Kigarama hadi wazazi wake walipolazimika kuhamia kijiji cha Gera ili aweze kusoma shule ya msingi. Hivyo, alisoma darasa la kwanza hadi la sita katika Shule ya Msingi Gera na kisha kwenda Shule ya Sekondari ya Nyakato kwa ajili ya Mafunzo ya Kilimo, ambapo alitunukiwa cheti cha ufundi kutoka Taasisi ya Kilimo Ukiligulu (Mwanza). Baada ya kuhitimu, alianza kufanya kazi kama afisa kilimo huko Bukoba.

Hapo awali, Kamuzora alikuwa Mlutheri mwaminifu, lakini kupitia darasa la kujifunza Biblia, alikuja kugundua kwamba siku ya kweli ya kupumzika haikuwa Jumapili, bali Jumamosi. Hata hivyo, wakati huo hakukuwa na taarifa zozote kuhusu kanisa lolote karibu au mtu mwingine yeyote aliyeabudu siku ya Jumamosi mkoani Kagera. Kwa hiyo, kwa miaka mitano mfululizo (1948 – 1952), Augustine Kamuzora angekaa peke yake ndani ya nyumba akisoma Biblia yake siku ya Sabato, akitumaini kwamba siku moja, watu wangegundua ukweli na kuungana naye katika kuabudu pamoja siku ambayo Biblia inasema imeandikwa kama siku ya kweli ya ibada.

Katikati ya 1952, mwalimu aliyeitwa Sosthenes Mtolela na mkewe walihamishwa kutoka shule ya Musoma na kupelekwa Shule ya Msingi Gera iliyopo Bukoba. Shule ilikuwa nusu kilomita kutoka nyumba aliyokuwa akiishi Mzee Kamuzora. Mwalimu huyu mpya alikuwa muumini wa Kanisa la Waadventista Wasabato kutoka Majita, Musoma, ambako watu wengi walikuwa Waadventista wa Sabato. Mwalimu huyu mgeni hakuionea haya Injili kama inavyoonyeshwa katika Jumamosi ya kwanza kabisa katika juma ambayo ndiyo tu alikuwa amefika katika kijiji cha Gera. Yeye na familia yake walichukua meza na viti, wakavipanga nje chini ya mwembe, na kuanza kuimba na kumwabudu Mungu. Kijiji kizima kilikuja kushuhudia “imani hii ya ajabu” ambayo hawakuwahi kuiona maishani mwao. Harakaharaka walimkimbilia Augustine Kamuzora na kumwambia kwamba mwalimu mpya ambaye alikuja “kijijini kwetu

anaabudu siku moja kama wewe, na labda uende kumwona.” Marehemu Mzee Kamuzora alikwenda mara moja na kukutana na Mwalimu Sosthenes Mtolela, ambaye alimweleza kwamba hakuwa peke yake katika ibada ya Mungu Jumamosi, na kwamba imani ya Waadventista Wasabato ni ya kweli na ndiyo imani pekee ya Biblia.

Sosthenes Mtolela alikwenda mbali zaidi na kumjulisha na kumtambulisha Augustine Kamuzora kwa mchungaji kiongozi wa Misheni ya Ikizu mjini Musoma na kumhimiza awasiliane naye ili aende huko kupokea mafundisho zaidi ya Waadventista Wasabato na hatimaye kubatizwa. Augustine Kamuzora alitafuta siku kadhaa za mapumziko kutoka kwa mwajiri wake, serikali ya Tanganyika, ili aweze kusafiri hadi Misheni ya Ikizu. Alipokea fundisho hilo la Sabato na akabatizwa mwaka wa 1952.

Augustine Lwehumbiza Kamuzora alioa mara mbili. Ndoa ya kwanza alifunga na Rahel Baikiliza (1917-1994), nayo ilifanyika mwaka 1939 katika Kanisa la Kilutheri la Kigarama. Kwa bahati mbaya ndoa hiyo ilivunjika mwaka 1946 kwa sababu Augustine Kamuzora aliamua kuwa Msabato kitu ambacho mke wake hakukubaliana nacho na hivyo kumuacha na kuolewa na mtu mwingine. Miaka sita baadaye, mwaka 1952, Mzee Kamuzora alimuoa Sara Rubairo (1927 – 2005), ambaye alikuwa mwalimu wa Biblia katika Misheni ya Bwasi huko Majita, Musoma. Katika maisha yake yote, Kamuzora alijaliwa kupata watoto saba, ambao ni Enock, Hezekia (1942-2016), Isaac, Israel, Miriam (1959-1999), Esther, na Anna.

Mikutano ya kwanza ya kambi kule Bukoba ilifanyika mwaka 1958. Augustine Kamuzora alilipia malazi na gharama za mikutano yote ya kambi.

## Uchungaji

Augustine Lwehumbiza Kamuzora alikuwa mwinjilisti mwenye nguvu na mkristo mcha Mungu. Shauku yake ilikuwa ni kuona kwamba mkoa wa Kagera unakuwa ngome ya Waadventista wa Sabato. Alitaka kuona eneo hilo linakombolewa kupitia mafundisho ya kweli ya Biblia. Alifanya kazi katika nyadhifa nyingi za kanisa, ikiwa ni pamoja na kutumika kama mzee, mjumbe wa Kamati Tendaji ya Union ya Tanzania (1974), na majukumu mengine mengi ya kanisa. Alikuwa mstari wa mbele katika uanzishaji na upandaji wa makanisa mapya katika wilaya za Bukoba, Karagwe, Muleba, Misenyi, Geita na Sengerema. Kwa hakika yeye ndiye aliyesimamia ujenzi wa jengo la Kanisa la Waadventista wa Sabato Bukoba na ujenzi wa nyumba ya mchungaji. Mnamo 1972, Union ilimteua kuwa mwangalizi wa fedha za ujenzi na michoro ya usanifu. Aliombwa kutafuta mkandarasi peke yake ambaye angejenga majengo hayo mawili. Alimchagua Yafes Kabyemela kujenga majengo hayo mawili mjini Bukoba. Zaidi ya hayo, alichangia sana kununua mashamba kwa ajili ya Kanisa. Alijitolea kununua kiwanja kwa ajili ya kanisa la Kyaka, Gera, Bishulo na Kanyigo.

Augustine Kamuzora alishiriki katika ujenzi wa makanisa karibu kila mahali alipozindua tawi jipya la Shule ya Sabato. Alijitoa mhanga wakati mwingi kwa kutumia

pesa zake ili kutegemeza kazi ya Mungu. Imani ya Waadventista Wasabato, ambayo ilijulikana kama “imani ya ajabu,” hapo mwanzo sasa imekuwa maarufu. Haya ndiyo yalikuwa maisha ya Kamuzora. Aliwaweka wainjilisti walei katika kila sehemu mpya ili kutunza mapya yaliyopangwa. Baadhi ya wainjilisti walei aliwategemeza hatimaye wakawa wachungaji. Wachungaji hao ni pamoja na Ibrahim Lwehinda, James Maliamungu, Simon Alex, Joseph Mungwabi, na wengineo.

Wakati fulani katika utumishi wake, alihamishwa na mwajiri wake kutoka Bukoba kwenda Geita. Alipofika huko alibaini kuwa hakuna sehemu hata moja Wilayani Geita ambapo watu walikuwa wakimuabudu Mungu siku ya saba ya juma. Alipata taabu ya kutafuta watu kutoka Musoma ( wajita ) ambao aliamini wanaweza kuwa Waadventista Wasabato kwa sababu Wajita wengi walikuwa Waadventista Wasabato. Dhana zake zilikuwa sahihi kwa sababu, kwa muda mfupi sana, aliibua idadi kubwa ya Waadventista wa Sabato katika mji wa Geita. Kwa kuwa hawakuwa na mtu wa kuwakusanya, hawakufikiria kukusanyika mahali pamoja siku ya Sabato kwa ajili ya ibada. Akawaalika nyumbani kwake, na wakaanza kuabudu huko kila Sabato. Idadi ya waumini ilizidi kuongezeka hadi akahisi kuna haja ya kuwaandikia barua Bupandagila (makao makuu ya Fildi ya Nyanza Kusini wakati huo), kuwaomba wamtume mchungaji ambaye angeweza kuandaa kanisa katika mji huo wa Geita. Kwa kuzingatia matakwa yake, Mchungaji Daudi Malyeta alitumwa mwaka 1965 kuandaa Kanisa la kwanza la Waadventista Wasabato mkoani Geita.

**Miaka ya Mwisho ya Kamuzora**

Augustine Lwehumbiza Kamuzora alistaafu utumishi wa umma Agosti 1966 akiwa na umri wa miaka 51. Alistaafu mapema kwa sababu alitaka kujikita zaidi katika uinjilisti na uanzishaji makanisa, jambo ambalo alilifanya kwa zaidi ya miaka 45 hadi kifo chake Jumamosi, Agosti 17, 2012. Kinondoni, Dar es salaam , Tanzania.

Kutokana na mchango mkubwa wa baba yao kwa Kanisa, watoto wake sasa wanahamasishana kuanzisha shule ya kumbukumbu ya baba yao nje kidogo ya mji wa Bukoba. Shule hii ikishajengwa, itatolewa kwa Kanisa na kuendeshwa na Kanisa.